



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA SHILINGI BILIONI 2.46 ZA UJENZI WA  
MIUNDOMBINU YA SHULE ZA SEKONDARI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, **Adv. Kiomoni Kibamba** anautaarifu Umma kuwa amepokea fedha kiasi cha **Tshs. 2,461,100,000.00 (Shilingi Bilioni 2.46)** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa na matundu ya vyoo katika shule **25** za Sekondari.

Kati ya fedha hizo **Tshs. 2,000,000,000.00 (Shilingi Bilioni 2)** ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mapya **80** katika shule **25** za sekondari na kila darasa limetengewa kiasi cha **Tshs 25, 000,000.00 (Shilingi Milioni 25)**.

**Shilingi milioni 187.5 (Tshs. 187,500,000.00)** zitatumika kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **15** katika shule **saba** za Sekondari za; **Nyasaka, Nyamanoro, Mwinuko, Kisundi, Kirumba, Kilimani na Sangabuye.**

**Shilingi Milioni 273.6 (Tshs. 273,600,000.00)** zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo **152** katika shule za sekondari **19**, na **kila tundu la choo litagharimu Shilingi Milioni 1.8 (Tsh. 1,800,000.00)**

Mkurugenzi kwa niaba ya uongozi wa Ilemela anatoa shukrani za dhati kwa **Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia Ilemela.

**Violencea S. Mbakile**  
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela**  
**24 Januari, 2024**

---

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,  
Tovuti: www.ilemelamc.go.tz